

Taswira Za Wanyama Katika Mashairi Ya Kezilahabi

Na

Dkt. Wael Nabil Ibrahim Othman

Profesa Msaidizi katika Idara ya Lugha za Kiafrika

Kitivo cha Lugha na Ufasiri – Chuo Kikuu cha Al-Azhar

Misri

2018

Iksiri

Makala hii inashughulikia taswira za baadhi ya Wanyama waliomo kwenye mashairi ya Kezilahabi, maana yake, na motifu alizozigusia kupitia taswira hizi. Kezilahabi ni mshairi na mtunzi maarufu wa riwaya na tamthilia, aliandika diwani tatu, nazo ni; Kichomi (1974), Karibu ndani (1988), na Dhifa (2008). Katika mashairi haya Kezilahabi ametumia taswira za wanyama wengi kwa umahiri mkubwa, kama vile; ng'ombe, mbwa, mbuzi, fahali, sungura, na mbwehe. Maswali ambayo makala hii inayaibua na kujaribu kuyajibu ni; wanyama waliotumika katika mashairi ya Kezilahabi wanaashiriwa maana gani? Na kupitia matumizi ya wanayama mshairi amegusia motifu gani?